kufanya kilimo biashara nchini mkoani Morogoro. Wa kwanza kushoto ni Meneja wa benki ya NMB Kanda ya Mashariki, Dismas Prosper. Benki ya NMB ilishiriki kama mdau wa kilimo nchini. (Na Mpigapicha Wetu)

# Mashamba darasa ya ufugaji samaki kuanzishwa nchini

**Na Edward Kondela, Morogoro**

SERIKALI imesema katika bajeti ya mwaka wa fedha 2021/22 ina mpango wa kuanzisha vituo vya ukuzaji viumbe maji katika halmashauri 80 za wilaya ikiwa na lengo la kuhakikisha kila halmashauri inakuwa na kituo hicho ambacho kitatumika kama shamba darasa kwa ajili ya kufundisha wananchi namna ya kufuga samaki.

Akizungumza juzi wakati Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji ilipotembelea kituo cha ukuzaji viumbe maji kinachozalisha vifaranga vya samaki cha Kingolwira kilichopo Mkoani Morogoro, Waziri wa Mifugo na Uvuvi Mashimba Ndaki amesema mkakati wa serikali kupitia vituo hivyo vitakavyokuwepo katika halshamauri zote za wilaya ni kuwa na samaki wengi wafugwao kwa njia mbalimbali ikiwemo ya mabwawa na kufikia uzalishaji wa samaki wa asilimia 50 kwa njia ya kufuga na asilimia 50 wanaotokana na maji ya asili.

"Kupitia tasnia hii ya ukuzaji viumbe maji tunataka kuweka nguvu kubwa ili tuweze kuvuna rasilimali ya uvuvi iweze kusaidia lishe, ajira na kuondoa umasikini kwa wananchi, hivyo wizara inaweka mikakati ya kuhakikisha inafikia malengo yake kupitia tasnia hii," alisema Ndaki.

Aidha, Waziri Ndaki alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi ina mpango wa kuhakikisha inavipa uwezo mkubwa na kuvikarabati vituo vyote vya ukuzaji viumbe maji vilivyopo nchini ili viweze kwenda sawa na uzalishaji wa vifaranga vya samaki kulingana na mahitaji yake.

Naye Mwenyekiti wa Kamati ya Kudumu wa Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji, Dkt. Christine Ishengoma ameipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuweka jitihada mbalimbali za kuhakikisha inazalisha kwa wingi vifaranga vya samaki pamoja na kutoa elimu juu ya ufugaji wa samaki.

Alisema kamati hiyo itaangalia vyema bajeti ya wizara itakayowasilishwa kwa ajili ya mwaka wa fedha 2021/22 ili iweze kuwa na tija na kuleta matokeo chanya hususan katika tasnia ya ufugaji samaki kwa kuwa bado ni eneo jipya ambalo watu wengi wanahitaji kujifunza na kujiingiza katika ufugaji huo.

Kwa upande wake Kaimu Mkurugenzi Msaidizi Idara ya Ukuzaji Viumbe Maji kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi Dkt. Imani Kapinga alisema kituo cha ukuzaji viumbe maji Kingolwira kilichopo Mkoani Morogoro, katika kutekeleza majukumu yake kati ya mwaka 2010 hadi 2020 kimetoa mafunzo kwa wananchi 11,280 kutoka mikoa mbalimbali pamoja na kuzalisha vifaranga vya samaki aina ya sato zaidi ya milioni sita vilivyosambazwa maeneo mbalimbali nchini.

Katika ziara hiyo, baadhi ya wajumbe wa Kamati ya Kudumu ya Bunge, Kilimo, Mifugo na Maji wameipongeza Wizara ya Mifugo na Uvuvi kwa kuhakikisha inakiboresha kituo cha Kingolwira kwa kufanya upanuzi wa baadhi ya majengo kwa ajili ya ukuzaji viumbe maji na kuiomba wizara izidi kufanya maboresho zaidi katika maeneo ambayo yanahitaji kufanyiwa kazi kufuatia ushauri mbalimbali uliotolewa na wajumbe hao.

MAJIRA UK 8.

Scanned with CamScanner



# Wito taasisi za utafiti kuwasaidia wafugaji

**Na Paul Mabeja,** MPWAPWA

NAIBU Waziri wa Mifugo na Uvuvi, Pauline Gekul, amezitaka taasisi za utafiti nchini kuwasaidia wafugaji ili waweze kufuga kisasa pamoja na kuzalisha mifugo yenye ubora na inayohitajika sokoni.

Kauli hiyo aliitoa wilayani hapa akiwa katika ziara kwenye Taasisi ya Utafiti wa Mifugo (TALIRI) Mpwapwa na Wakala wa Mafunzo ya Mifugo (LITA) Mpwapwa.

Naibu Waziri Gekul, alisema taasisi hizo zinatakiwa kusambaza mbegu bora, pamoja na kuwajengea uwezo wa kufuga ili waweze kufuga kisasa na hatimaye kujiingizia kipato.

Alisema Wizara ya Mifugo na Uvuvi inagusa kundi kubwa la Watanzania kutokana na wengi kufuga hivyo taasisi hizo zinawajibu wa kuwasaidia kufikia ndoto zao.

Pia aliwataka kuyatumia maeneo makubwa ambayo wanayo kwani yamekuwa yakichochea migogoro kati yao na wafugaji.

"Nimetembea katika taasisi hizi, lakini tatizo kubwa ni kuwa na maeneo makubwa ambayo hamyatumii na hivyo huchochea migogoro kati ya jamii inayo wazunguka na halmashauri wamekuwa wakizidi kuiomba na kuitumia ardhi hiyo sasa lazima ardhi mliyonayo muitumie kwa manufaa hamuwezi kuwa na ardhi hekta 8,000 lakini kuwa na ng'ombe 700 hii haikubaliki," alisema.

Pia aliutaka uongozi wa Taliri Mpwapwa kulipa madeni ya vibarua wanaoidai taasisi hiyo ndani ya miezi mitatu.

Kwa upande wake, Mkurugenzi wa Utafiti, Mafunzo na Ughani kutoka Wizara ya Mifugo na Uvuvi, Dk. Angelo Mwilawa, alisema moja ya majukumu ya taasisi hiyo ni kutafiti ng'ombe wa maziwa na wa nyama aina ya Mpwapwa Breed.

"Tunalenga zaidi kuhifadhi aina ya ng'ombe hao ambao wameonekana kufanya vizuri kwa ufagaji wa Tanzania," alisema.

Alisema taasisi hiyo ipo kwenye majaribio ya kuzalisha ng'ombe kwa kutumia viini tete ambavyo husaidia kupata ng'ombe wengi kwa muda mfupi.

Mkuu wa Wilaya ya Mpwapwa, Jabir Shekimweri, alisema taasisi hizo zinatakiwa kufanya utafiti unaolenga kumnufaisha Mtanzania wa chini ili apate faida katika ufugaji wake.

"Lazima taasisi za Mpwapwa zitumie fursa ya makao makuu Dodoma kuweza kuzalisha kwa wingi bidhaa za mifugo kama maziwa, kuku na kuwa na bucha za kisasa ambazo zitakuwa chanzo cha mapato kwa taasisi hizo na hivyo kiziwesha kujiendesha na kupunguza utegemezi kwa serikali.



# BURIANI RAIS DKT. JOHN MAGUFULI -19

## MIAKA 6 YA HAYATI RAIS MAGUFULI




Scanned with CamScanner